

# JOYCE MEYER



NISAIDIE -  
NINAOGOPA!

KUSHINDA VITA VYA HISIA KWA  
KUTUMIA NGUVU ZA NENO LA MUNGU!

# NISAIDIE - NINAOGOPA!

---

Kushinda Vita vya Hisia kwa Kutumia Nguvu za neno la  
Mungu

**JOYCE  
MEYER**



**JOYCE MEYER**  
MINISTRIES

P.O. Box 5, Cape Town 8000

Maandiko yote yaliyoonyeshwa ila tu unapoelezwa, yametolewa katika Tafsiri ya Habari Njema ya Biblia.

Maandiko yaliyo na alama (UNION) yametolewa katika Biblia ya Tafsiri ya UNION.

English copy

*HELP ME – I'M AFRAID!*

*Overcoming Emotional Battles*

*With The Power of God's Word*

ISBN 1-57794-035-0

Copyright © 1998 by Joyce Meyer

Joyce Meyer Ministries

P.O. Box 655

Fenton, Missouri 63026

USA

Swahili Translation

*NISAIDIE – NINAOGOPA!*

*Kushinda Vita vya Hisia kwa Kutumia*

*Neno la Mungu*

Nairobi Lighthouse Church

P.O. Box 34041-00100

Nairobi, Kenya

# YALIYOMO

*Utangulizi*



Sehemu ya 1 - Uhuru Kutokana na Hof

1. Kukabiliana Na Hofu
2. Omba Kuhusu Kila Kitu Usiogope Chochote
3. Aina Ya Maombi
4. Funguo Za Ufalme

Mwishowe

Sehemu ya 2 - Maandiko

- Maandiko Ya Kushinda Hofu
- Ombi la Kukabiliana na Hofu
- Ombi la Kuwa na Uhusiano wa Karibu na Bwana

Kuhusu Mwandishi

# UTANGULIZI



Moja ya faida nyingi ambazo tunazo kama waamini ndani ya Yesu Kristo, ni uhuru kutokana na hofu. Lakini hata kama tunahofu, tunaweza kuendelea mbele na kutenda yaliyo mbele yetu, kwa sababu Mungu atakuwa nasi na atatulinda. Atatusaidia, yeye ataenda mbele yetu na kutupigania na kutukomboa iwapo tutamtii.

Iwapo unahisi kana kwamba umekosa mambo fulani katika maisha yako kwa sababu ya hofu, unaweza kujifunza kushinda hofu na uanze kuhisi uzima teletele ambao Mungu amekutayarishia.

**Sehemu ya 1**

**Uhuru Kutokana na Hof**

# 1



## KUKABILIANA NA HOFU

*...Bwana Mungu anayekwenda mbele yenu, hatawaacha wala kuwapungukia.*

*Kumbukumbu 31:6*

Ujumbe huo, “Usiogope, kwa maana Mimi Mungu, niko pamoja nawe,” umeashiriwa mara nyingi sana katika Biblia. Mungu hataki tuishi kwa hofu kwa maana hofu hutuzuia kupokea na kufanya yote ambayo Mungu ametupangia. Anatupenda na anataka kutubariki na amefanya njia kwetu tuweze kuishi bila hofu.

Tunaweza kuona katika maandiko haya yafuatayo kwamba wale wanaomwamini Yesu hawahitaji kuogopa mambo ambayo wasioamini—watu “wa ulimwengu”—wanayoogopa. Mungu hataki tuogope mambo hayo.

Mwenyezi Mungu alinionya kwa nguvu nisiifuate njia za watu hawa, akaniambia, “Usijumuike nao katika njama zao, wala usiogope yale wanayoyaogopa wala kuwa na hofu. Nitambue mimi peke yangu, Mwenyezi Mungu wa majeshi, kuwa mtakatifu; utaniogopa na kunicha mimi peke yangu.

*Isaya 8:11-13*

Katika neno lake, Mungu anatuambia kwamba tunaweza kuishi kwa ushindi, tukiwa wenye nguvu ndani yake na uweza wake. Yeye ametuahihidi kuwa hatatuacha au kutupungukia hata iweje.

### ***Hakuna hofu!***

Kila mmoja wetu amehisi hali ya kujaribu kuanza kutembea kwa imani, lakini kila unapoanza kufikiria juu yake, hofu inakubana. Tunahitaji kutambua kuwa chanzo cha hofu ni Shetani. Yohana wa kwanza 4:18, inasema;

Palipo na upendo hapana uoga; naam, upendo kamili hufukuza uoga wote. Basi, mtu mwenye uoga hajakamilika bado katika upendo, kwani uoga huhusikana na adhabu.

Shetani hututumia hofu akijaribu kututesa ili tujae mashaka na huzuni kiasi cha kutoweza kufanya na kupokea yote ambayo Mungu ametutayarishia.

Tunaweza kuishi bila hofu kwa kujenga imani yetu juu ya yale Mungu amesema katika neno lake. Kwa mfano:

Maana Mungu hakitupa roho ya woga, bali ya nguvu na ya upendo na ya moyo wa kiasi.

*2 Timotheo 1:7 (UNION)*

Iweni hodari na moyo wa ushujaa, msiogope wala msiwahofu; kwa maana BWANA, Mungu wako, yeye ndiye anayekwenda pamoja nawe, hatakupungukia wala kukuacha.

*Kumbukumbu 31:6 (UNION)*

Warumi 10:17 inatuambia hivi; “Hivyo basi, imani inatokana na kuusikiliza ujumbe, na huo ujumbe unatokana na neno la Kristo.” Tunahitaji kujifunza na kulikiri neno la Mungu, hasa maandiko kama haya na yale yaliyo mwisho wa kitabu hiki na tuyanywe kama tuyanywavyo maji wakati tunaona kiu. Tunapofungua



vinywa vyetu na kukiri neno la Mungu juu ya maisha yetu na hali zetu, neno la Mungu litatupatia nguvu za kushinda kila hofu inayotutesa na kutuzuia.

Na sisi tuko thabiti mbele ya Mungu kwani tuna hakika kwamba tukimwomba chochote kadiri ya mapenzi yake, yeye hutusikiliza. Yeye hutusikiliza kila tunapomwomba; na kwa vile tunajua kwamba yeye hutusikiliza kila tunapomwomba, twajua pia kwamba atupatia yote tunayomwomba.

*1 Yohana 5:15*

Kuna nguvu katika kulikiri neno la Mungu katika maombi. Ninaamini hii ni mojawapo ya mambo muhimu kabisa tunayoweza kufanya katika maombi, kulikiri neno la Mungu.

Wakati tunapojikuta tunajaribu kuepuka kusuluhisha jambo fulani kwa sababu ya hofu na woga au mawazo mengi, tunafaa kuomba na kumwuliza Mungu atufanyie yale ambayo ametuahidi katika neno lake—atutangulie mbele na atufanyie njia. Yakobo anatufundisha kwamba hatuna kwa sababu hatuombi. (Yakobo 4:2) Yesu anatuambia tuombe, tutafute na tubishe. (Mathayo 7:7).

Kwa mfano; wakati tunapotazamia kufanya mtihani wa kupata kazi, badala ya kuogopa kwamba tutakosea na tuishie kuanguka, tunaweza kumwomba Mungu awe pamoja nasi na tuamini kwamba yeye ataenda mbele yetu na kutufanyia njia ili tuweze kujieleza kwa njia bora na ifaayo. Kisha tunaweza kumtegemea kwamba chochote kitakachotokea, mambo yote yatafanyika kwa ajili ya kuleta mema maishani mwetu kulingana na mpango wa Mungu juu ya maisha yetu.

### ***Tenda Uoga Ungalipo!***

Bwana alimtokea Abram u kule Harani na kumwambia, inuka, toka katika nchi yako na nyumba ya baba yako katika nchi ambayo

nitakuonyesha.

*Mwanzo 12:1*

Je, utasikiaje iwapo Bwana angekuambia uache nyumba yako, jamii yako, na kila kitu ambacho unakifahamu na uelekee katika nchi usiyojua? Utakuwa umejawa na hofu?

Hii ndio changamoto aliyopata Abram u katika maandiko haya—naye alitishika. Hii ndio sababu Bwana aliendelea kumtokea na kumwambia tena na tena, “Usiogope.”

Huu ndio ujumbe ule ule ambao Bwana alimpa Yohana alipomwita awaongoze wana wa Israeli kuitaka nchi ambayo alikuwa amewaahidi kupokea kama urithi wao (Yohana 1:6,7,9).

Mtu ambaye anamfanyia Mungu jambo lolote atahitaji kumsikia Bwana akimwambia tena na tena, “Usiogope.”

Elisabeth Elliot, ambaye mume wake aliuwawa pamoja na wamishenari wengine wanne nchini Equador, anasema kuwa maisha yake yalitawaliwa na hofu na woga. Kila wakati alipojaribu kufanya chochote, hofu ilimzuia. Rafiki yake alimwambia jambo ambalo lilimweka huru. Alimwambia, “Kwa nini usifanye jambo hilo ukiwa na hofu?” Elisabeth Elliot pamoja na Rachel Saint, ambaye alikuwa ni dada ya mmoja ya wamishenari ambao waliuawa, walijitoa na wakaenda kuwahubiria wahindi wa kabila lile, wakiwemo watu wale waliokuwa wamewaua mume wa Elisabeth na kakake Rachel.

Mara nyingi sisi husubiri mpaka tunapokuwa hatuhisi hofu ili tuweze kufanya jambo. Iwapo tutaishi hivi, basi ni machache sana tutaweza kutimiza kwa ajili ya Mungu, wengine na katika maisha yetu wenyewe. Iliwabidi Abram na Yohana wapige hatua ya imani na watende yale ambayo Mungu alikuwa amewaambia—huku wakiwa na hofu.

Mungu alinikumbusha hadithi hiyo ya Elisabeth, “Fanya—hata

ukiwa mwenye hofu” na kisha akaanza kunionyesha mambo fulani kuhusu hofu na woga.

### ***“Usiogope” Humaanisha “Usikimbie”***

Msiogope; simameni imara nanyi mtauona ukombozi wa Bwana ambao atawafanyia leo.

*Kutoka 14:13*

Mungu alinionyesha kutokana na maandiko haya kwamba maneno hayo, “Usiogope”, humaanisha “Usikimbie”. Suluhisho la hofu nalo ni rahisi. Wakati tunapokumbwa na hofu, badala ya kuiinamia na kuikubalia, tunafaa kusimama kinyume chake na tufanye kile tunachoogopa.

Hayo ndiyo Mungu anayotuambia katika neno lake. Hata kama tunatetemeka, magoti yetu yanayumbayumba, kinywa chetu ni kikavu, na tunahisi ni kama tutaanguka chini, tunahitaji kuendelea kusema, “Bwana, nipe nguvu. Haya ndiyo umeniambia nifanye, na kwa msaada wako, nitayafanya, kwa sababu huu ni ufunuo wako kwa ajili yangu. Nimeamua kuwa maisha yangu hayatawaliwa na hofu bali na neno lako.

### ***Kabili Hofu Kwa Neno La Mungu***

Huwezi kutamani kwamba hofu iondoke nayo iondoke, ni lazima ikabiliwe na kuondolewa kwa neno la Mungu.

Kuna nyakati ambazo watu wamekombolewa kutokana na hofu kwa kupitia muujiza wa maombi. Mimi sikatai haya. Ni kweli tunamtumikia Mungu afanyaye miujiza. Kuna watu kadhaa ambao nimewaombea wakombolewe kutokana na hofu na wamekuja kwangu baadaye na kuniambia, “Baada yako kuniombea, sijawahi kutatizwa au kufungwa na hofu tena.” Lakini mara nyingi, sisi hushinda hofu kwa kulitafakari na kulizungumza neno la Mungu

na kuipinga hofu kwa nguvu za Roho Mtakatifu.

Mimi mwenyewe nilikuwa na shida nyingi kwa sababu ya kunajisiwa nilipokuwa ningali mdogo. Nilikuwa na maeneo mengi ya maisha yangu ambayo yalihitaji ukombozi. Ni sehemu moja tu ambayo Bwana alinikomboa kwa muujiza. Kila ukombozi mwingine nilioupata ulitokana na kulitumia neno. Mara nyingi, Mungu hutuwezesha 'kupitia' shida zetu badala ya kutukomboza ghafla kutoka kwa shida hiyo.

### *Hofu ni Uongo*

...ibilisi, alikuwa muuaji kwanzia hapo mbeleni na hakuna kweli ndani yake. Anaposema uongo, yeye huwa anazungumza lugha yake ya kawaida, kwa maana yeye ni mwongo na baba wa uongo wote.

*Yohana 8:44*

Biblia haisemi "Usitetemeke" au "Usiyumbayumbe" au "Usitokwe jasho", inatumbia, "Usiogope." Kuna tofauti kati ya maneno hayo.

Katika mfano niliopeana, kuogopa ni kukimbia au kutoroka kitu. Rafiki yake Elisabeth Elliot alikuwa anamwambia Elisabeth aanze kufanya kile alichokiogopa badala ya kukikimbia.

Inasemekana kwamba uoga ni mambo ya uongo yanayoonekana kana kwamba ni ya kweli.

Yesu alisema kuwa shetani ni mwongo na baba wa uongo wote. Hakuna ukweli ndani yake. Yeye hujaribu kutumia hofu kuwadanganya watu wa Mungu waishi kwa hofu ili wasiweze kuwa shujaa na watiifu na wapate baraka alizowakusudia Mungu maishani mwao.

Mara nyingi, hofu yetu huwa kubwa kuliko kitu tunachokihofia. Iwapo tunaweza kuwa shujaa na wenye moyo na tuamue kufanya tunachokiogopa, basi tutagundua kwamba jambo hilo si gumu

kama tulivyoogopa.

Katika Biblia, tunaona mara kwa mara Mungu akiwaambia watu wake, “Msiogope.” Ninaamini sababu yake kuwaambia hivi ilikuwa kuwahimiza ili wasimkubalie shetani aibe baraka zao.

Vivyo hivyo, kwa kuwa Mungu anajua kwamba sisi hupatwa na hofu, yeye hutuhimiza na kutuita tukaze mwendo kufikia yote yaliyo mbele yetu na yale ambayo ametuambia tufanye. Kwa sababu gani? Kwa sababu anajua kwamba kuna baraka kuu zinazotungoza tukisha yapitia yale yanayojaribu kutuzuia.

Tunaona mfano wa haya katika maisha ya Abramuu.

### ***Ushujaa Na Utiifu Yana Zawadi Kuu***

Baada ya haya, neno la Bwana likamjia Abramuu katika maono, likisema, usiogope, Abramuu, mimi ni ngao yako na tuzo lako.

*Mwanzo 15:1*

Kama tulivyoona katika mwanzo 12:1, Mungu alimwamrisha Abramuu afanye jambo gumu kweli. Kwa maneno mengine, yeye alimwambia, “Funga virago vyako na uachane na kila kitu na kila mtu ambaye unafahamiana naye hapa uelekee mahali ambapo nitakuonyesha.”

Kwa njia ileile, kama Yoshua hangeishinda hofu yake na awe mtiifu kwa amri ya Bwana ya kuwaongoza wana wa Israeli kuingia katika inchi ya ahadi, yeye na hata wao hawangeweza kuyafurahia yale ambayo Mungu alikuwa tayari amewatayarishia.

Kuna nguvu katika neno la Mungu ambazo zinaweza kutuwezesha tusiinamie hofu ya shetani na tamaa zake. Tunaweza kufanya yale ambayo Mungu ametuamuru tufanye hata kama tutayafanya kwa hofu.

# 2



## OMBA KUHUSU KILA KITU USIOGOPE CHOCHOTE

*... Sala ya mtu mwema ina nguvu ya kutenda mengi...*

*Yakobo 5:16*

Wakati mmoja, Bwana alinizungumzia maneno haya; “Omba kuhusu kila kitu, na usiogope chochote.” Aliniambia hivi nilipokuwa na hofu kwamba msukaji nywele ambaye nilikuwa nimemwendea kwa mara ya kwanza hangeweza kutengeneza nywele zangu vizuri.

Roho Mtakatifu alinizungumzia, “Usiogope hali hii, wewe iombe. Omba kwamba Bwana atampa upako mwanamke huyu ili aweze kufanya kile kinachohitajika.”

Kisha katika majuma yaliyofuatia, Bwana aliendelea kunionyesha mambo tofauti kuhusu vile maombi yanavyoishinda hofu. Mengi yao yalikuwa ni maeneo madogo madogo ambayo hofu hujaribu kuingia na kuniletea shida. Alinionyesha kuwa katika kila hali, haijalishi ukubwa au udogo wake, suluhisho la hali hiyo lilikuwa ni maombi.

Usiogope, kwa maana ni pamoja nawe; usiangalie huku kule kwa hofu na kutahayarika, kwa maana mimi ni Mungu wako. Nitakupa nguvu wakati wa magumu, nitakusaidia. Nitakuinua

kwa mkono wangu wa kuume...

*Isaya 41:10,13*

Katika maandiko haya, Bwana anawaambia watu wake wasiangalie huku na huko wakiwa na hofu au wasiwasi, kwa maana yeye ni Mungu wao.

Wakati mwingine sisi huogopa tunapoangalia hali ambayo tumo ndani yake. Haya ni makosa. Jinsi tunavyoendelea kukaza macho yetu na midomo yetu kwenye shida, ndivyo tunavyoendelea kushikwa na hofu. Badala yake, tunafaa kuweka macho yetu na midomo yetu juu yake Mwenyezi—Mungu. Yeye anaweza kutatua lolote ambalo litawahi kutujia katika maisha haya.

Mungu ameahidi kutupatia nguvu, na kutuimarisha katika magumu, kutuina na mkono wake wa kuume. Anatuamrisha pia tusiwe na hofu. Lakini kumbuka, yeye hatuamrishi tusihisi hofu au woga, bali tusikubalie hofu au woga ututawale.

Mungu anatuambia mimi na wewe, “Usiogope, nitakusaidia.” Lakini hatuwezi kuupokea msaada wa Mungu mpaka tutakapojiachilia na tuwe watiifu na kutenda atuambialo kwa imani.

Je, unajua ni wakati gani ninahisi upako wa kuhubiri? Ni wakati ninapopanda jukwaani nianze kuhubiri—si kabla yangu kuanza.

Mungu anatuambia leo, “Acha kukubalia hofu itawale maisha yako. Anza kufanya yale ninayokuambia ufanye, kwa maana ninayokuambia ni kwa faida yako mwenyewe. Ninajua baraka zilizo ng’ambo ya pili, lakini ibilisi pia anazijua. Hii ndio sababu anakupinga kwa hofu na ndio sababu mimi ninakuambia usiogope.”

### ***Usiogope, Wewe Ni Wangu!***

...hivyo asema Bwana, aliyekuumba, Ee Israeli, aliyekutengeneza

Ee Yakobo; usiogope kwa maana nimekukombo; nimekuita kwa jina lako, wewe ni wangu.

Utakapopita kwenye maji, nitakuwa nawe; utakapopitia mito, haitakugharikisha. Utakapopita kwenye moto, hutachomeka, na miali ya moto haitakuunguza.

*Isaya 43:1,2*

Bwana anatuambia hapa tusiogope wakati tunapopitia majaribu ya kila aina. Hii inamaanisha kwamba tutapata ushindi katika maisha yetu, lakini itakuwa ni wakati tunapopitia mambo hayo. Kuweza kupitia mambo hayo, ni lazima tuamue kwamba hatutakimbia mbele ya majaribu tena.

Bwana ameahidi kuwa nasi na kutuweka salama wakati tunapopitia maji mengi ambayo hayatatugharikisha na tunapopitia moto ambao hutatuunguza au kutuchoma.

Je, unaikumbuka hadithi ya wale vijana watatu wa Kiebrania walioitwa Shadraka, Meshaki na Abednego? Walitupwa katika tanuru ya moto mkali lakini hawakuumia hata. Hawakuwa hata na harufu ya moto. (Danieli 3:1-30).

Kuna hofu za kutisha, kama ya kutupwa katika tanuru la moto—na kuna hofu ndogo ndogo, kama kuogopa kwamba nywele yako haitatengezwa vizuri!

Unaweza kuwa unaogopa kitu kikubwa kama vile Kansa au mshtuko wa moyo au kifo cha mpendwa katika jamii. Au unaweza kuwa unaogopa kitu kidogo kama mvua wakati wa matembezi au kukosa mahali pa kuegesha gari lako.

Haijalishi chanzo au ukubwa wa hofu yako, ni lazima hofu hiyo itatuliwe kwa njia ile ile. Kama tulivyoona, ni lazima ikabiliwe kwa maombi na neno la Mungu. Na wakati tunapoomba, ni lazima tuamini. Hofu ni adui yetu na tunafaa kuichukua kuwa adui.



## ***Imani: Dawu Dhidi ya Hofu***

Lakini kama mmoja wenu amepungukiwa hekima, basi, anapaswa kumwomba Mungu ambaye atampatia; kwani Mungu huwapa wote kwa wingi na kwa ukarimu.

Lakini anapaswa kuomba kwa imani bila mashaka yoyote. Mtu aliye na mashaka ni kama mawimbi ya bahari ambayo husukumwa na kutupwatupwa na upepo.

Mtu wa namna hiyo, mwenye nia mbili na asiye na msimamo katika mwenendo wake wote, asidhani anaweza kupata chochote kutoka kwa Bwana.

*Yakobo 1:5-7*

*Imani ndio kinga ya kipekee dhidi ya madhara mabaya ya hofu.*

Iwapo mtu amekunywa aina fulani ya sumu, basi itambidi ameze kizuia madhara au dawa dhidi ya sumu ile la sivyo, sumu ile inaweza kumdhuru sana au hata kusababisha kifo. Hivi ndivyo ilivyo na sumu mbaya ya hofu. Ni lazima uwe na dawa ya kuizuia, na dawa yake ya pekee ni imani.

Hofu inapobisha mlangoni, ni lazima tuitikie kwa imani, kwa maana hakuna kitu kingine kinachoweza kuishinda. Na maombi ndio gari linaloibeba imani.

Ni lazima imani isafirishwe kwenye shida na iachiliwe kwa njia moja au nyingine. Tunaweza kuomba bila imani (wengi wetu hufanya hivi kila wakati), lakini huwezi kuwa na imani ya kweli nawe ukose kuomba.

Yakobo anatuambia kwamba tunapojikuta tukiwa na hitaji fulani, tunafaa kumwomba Mungu kwa maombi rahisi na ya imani. Maneno hayo mawili ni muhimu sana. Tunafanya hivi kwa kuomba kwa imani, tukiamini kwamba tutapokea yale tuliyoomba kulingana na mpango na makusudi ya Mungu.

Kwa hiyo ufunguo wa kushinda hofu ni rahisi, Maombi yaliyojaa imani, bila kukoma.

### ***Ombeni kila wakati!***

Salini daima, mkiomba msaada wa Mungu. Salini kila wakati kwa nguvu ya Roho. Kesheni bila kuchoka mkisali kwa ajili ya watu wote wa Mungu.

*Waefeso 6:18*

Katika Waefeso 6:10-17, Mtume Paulo anazungumza kuhusu silaha za Mungu na jinsi tunavyoweza kuzitumia pamoja na silaha ya neno la Mungu katika vita vya kiroho. Baada ya kuzitaja sehemu zote za silaha hizo, Paulo anamalizia ujumbe wake kwa kusema, “Salini daima...” Tunafaa kuomba wakati gani? Kila wakati. Tunafaa kuomba vipi? Katika Roho, tukitumia kila aina ya maombi. Katika sura ifuatayo tutaangalia aina tofauti za maombi, lakini sasa hivi, hebu tutazame maana ya “Kuomba daima.”

Hii inamaanisha nini? Je inamaanisha kuwa hata kama tunanunua vitu dukani na Mungu atupatie mzigo wa kuomba tunafaa kupiga magoti pale pale katikati ya duka na tuanze kuomba?

Mara nyingi mimi hupiga magoti kando ya kitanda changu ili nipate kuomba. Kuna nyakati zingine ambapo nitahisi Mungu akiniongoza nilale chini kifudifudi, mbele yake katika maombi. Tunahitaji kutofautisha kati ya maombi, na jinsi tunavyojipinda wakati tunapoomba. Tunaweza kuomba kimoyomoyo pale dukani tunapoendelea kununua vitu.

Katika vipindi tofauti vya maisha yetu, tuna uwezo wa kuomba kwa njia tofauti. Mama mchanga ambaye ana watoto watatu au wanne wadogo, atawajibika kupanga maisha yake ya maombi tofauti na nyanya ambaye amestaafu na watoto wake wamekua na kuondoka nyumbani.

Tukifanyika “watu wa kidini” sana kuhusu swala la maombi, tukifikiri tunafaa kuomba kwa njia fulani kwa sababu hivyo ndivyo fulani wa fulani anavyoomba, tutaishia kuhukumika. Jambo la muhimu kuhusu maombi si vile ulivyojipinda au mahali au wakati wa kuomba bali ni kuomba kwa imani—kila wakati, bila kukoma. Kila wakati unapohisi kuomba au hitaji linapotokea... OMBA!

### ***Ombeni Bila Kukoma***

Salini kila wakati...

*1 Wathesalonike 5:17*

Tafsiri zingine zinatafsiri mstari huu kusema hivi: “Ombeni bila kukoma.”

Nilikuwa ninayasoma maneno hayo na kujiuliza, “Bwana, ninawezaje kufika mahali ambapo ninaomba bila kukoma?” Katika mawazo yangu, bila kukoma ilimaanisha kuendelea bila kuacha au kupumzika.

Sikuelewa haya yangewezekanaje.

Lakini sasa ninaelewa maana ya maneno haya ambayo Paulo alikuwa akisema. Alimaanisha kuwa maombi yanafaa kuwa kama kupumua, jambo ambalo sisi hufanya kila wakati hata ingawa haliko katika mawazo yetu.

Mimi na wewe tunaishi kwa kupumua. Miili yetu inahitaji hewa ili iendeleo kuishi. Hivyo ndivyo ilivyo na roho zetu, zinalishwa na kukuzwa na maombi.

Shida ni mawazo ya kidini yanayosema kwamba iwapo hatufuati mpango fulani wa maombi, basi sisi tunakosea. Sisi tunajizoeza kulinganisha maombi, na masaa ambayo tunatumia kuomba.

Mungu alinipa mfano huu kunionyesha jinsi tunapaswa kuomba.

Jinsi tunavyopumua siku nzima, bila ya kutumia muda tukihesabu tumepumua mara ngapi, ndivyo tunavyopaswa kuomba siku nzima bila ya kuhesabu tumeomba mara ngapi.

Sijawahi kubeba saa ili nione nitapumua mara ngapi kila nukta. Sijawahi kutoka kazini na kuingia nyumbani na kuandika katika kitabu changu nilipumua mara ngapi katika siku hiyo. Ninapumua kila ninapohitaji, bila ya kukoma, bila ya kuyawazia sana mambo haya. Hivyo ndivyo tunavyopaswa kuwa katika maombi yetu.

Sijui mimi huomba mara ngapi kwa siku moja; mimi huomba siku mzima. Ninaanza kuomba ninapoamka asubuhi na ninaendelea kuomba hadi ninapoenda kulala usiku. Mimi hufurahia nyakati ambazo nimezitenga kando ili nipate kuomba lakini mimi huomba nyakati zingine pia.

Je, hii inamaanisha kwamba mimi sifanyi jambo lingine lolote? La. Kuna nyakati ambazo ninajitoa kufanya mambo mengine.

Lakini tutakapoanza kuona aina tofauti ya maombi, tutaona kwamba tunaweza kuomba kila wakati, kila majira, kila mahali, na kwamba Mungu atasikia maombi hayo—ambayo ni muhimu na yenye nguvu sawasawa na maombi mengine tunayoomba.

Je, unajua ni kwa nini shetani anataka tujihisi kuhukumika kuhusu ya maisha yetu ya maombi? Anajua kwamba iwapo anaweza kutufanya tujihisi hatuombi ipasavyo, basi tutaomba ili tu tutimize jukumu la kuomba, lakini hatutakuwa tukiachilia imani tunapofanya hivyo; na maombi kama haya hayatufaidi kitu.

### ***Kanuni za maombi***

Petro na Yohana walikuwa wanakwenda hekaluni katika saa ya maombi...

*Matendo 3:1*

Kuna watu wengi ambao hawapendezwi na maisha yao ya

maombi. Hakuna haja ya kuhisi hivi kwa sababu kila mtu ana maisha yake ya maombi ambayo ni tofauti na ya mwingine. Na si lazima maisha ya watu wawili tofauti yafanane.

Ni kweli kuna kanuni fulani za maombi ambazo zinastahili kufuatwa. Ni vyema kwa mfano, kujitia nidhamu kuwa na wakati na mahali maalum pa maombi.

Hata katika agano jipya, kama tunavyoona katika kitabu cha Matendo, wanafunzi wa Yesu walikuwa na masaa fulani ambayo walikuwa wameyatenga ambapo walienda mahali maalum kwa ajili ya maombi. Huo ni mtindo mwema wa kuwa nao, lakini hufai kuwa mwanzo na mwisho wa maombi.

Ukweli ni kwamba tunafaa kujitia nidhamu na tuthibitisha mpango maalum wa maombi ambao unatufaa sisi na tuushikilie mpaka uwe sehemu ya maisha yetu ambayo tunaifanya hata bila ya kuwaza.

Kulikuwa na wakati ambapo ilinibidi nijitie nidhamu kupiga mswaki. Lakini sasa nimejifunza na kufanya hivyo kwa muda mrefu kiasi cha kwamba sihitaji kuwaza na kufikiri juu yake. Ni jambo la kawaida kwangu. Ninapiga mswaki kabla ya kwenda kulala usiku, ninapoamka asubuhi na baada ya kila mlo. Kupiga mswaki sasa ni sehemu ya kawaida ya maisha yangu ya kila siku.

Funzo hilo ni la kweli pia kuhusu kutembea na Bwana. Mwanzoni yawezekana kuwa tunahitaji tujitie nidhamu katika maeneo mengine ya maisha yetu kwa sababu hatukuwa na nidhamu yoyote katika maeneo hayo. Lakini baada ya muda, mambo haya yanafaa kuwa sehemu ya kawaida ya maisha yetu kiasi ya kwamba tunayafanya bila ya kuyafikiria.

Ninaamini kuwa iwapo tutamkubalia, Roho Mtakatifu atatuongoza katika maombi bila ya kukoma hadi iwe ni kama kupumua. Jambo hilo likifanyika basi tutakuwa tunaomba bila kukoma.

Tunaweza kuamka asubuhi na kusema, “Hujambo Bwana,

ninakupenda.” Tunaweza kwenda mezani kula kiamsha kinywa na kusema, “Baba, wewe ni mwema kwangu sana.” Tunaweza kuelekea kazini tukisema, “Asante Bwana, kwa mambo yote mema ambayo utanifanyia leo.”

Siku nzima, na hata jioni, tunaweza kuendelea kuwasiliana na Bwana, tukimsifu na kumwabudu, tukimshukuru kwa sababu ya uwepo wake na kuomba msaada wake tunapopatwa na shida yoyote. Kabla ya kwenda kulala, tunaweza kumpa ombi la mwisho la shukrani kwa sababu ya baraka zake na kumwomba usingizi mwema.

Shetani anaweza kuanza kukuambia kwamba huko si kuomba kwa sababu hujakaa au kujipinda kwa njia fulani wala kutumia lugha ya “kikanisa”. Huu ndio wakati wa kumpiga shetani mweleka! Ni wakati wa kumnyamazisha kwa sababu maombi si jambo la kimwili au kimaneno tu, bali yanahusisha roho, nia na mioyo yetu.

Na mahali palipo na maombi pana nguvu!

### ***Maombi Ni Nguvu!***

...Sala ya mtu mwema ina nguvu ya kutenda mengi.

*Yakobo 5:16*

Maombi rahisi yalioombwa kwa imani yana nguvu! Hakuna kitu chenye nguvu kama maombi yanayoombwa na moyo mkunjufu, tukiomba bila kukoma!

Sababu ya shetani kututesa kuhusu maisha yetu ya maombi na kujaribu kutuzuia tusiwe waaminifu kuomba ni kuwa anataka tuwe dhaifu. Anajua kwamba tukiendelea katika maombi yaliyojaa imani, basi tutaharibu nguvu zake na kusababisha mapenzi ya Mungu yafanyike hapa duniani.

Wakati wowote tunapoanza kuhisi kuhukumika kwa sababu ya maisha yetu ya maombi, basi tunaanza kupoteza uwezo wetu wa kuiachilia imani katika maombi. Ili tuweze kukamilisha yale ambayo Mungu ametuitia kufanya katika maisha haya, tunahitaji kuwa na uhakika kwamba anasikia maombi yetu na anayaitikia. Imani hii ndio inayapa maombi yetu nguvu kuu.

Hii ndio maana tunahitaji kuacha kuogopa na tuanze kuomba—kwa imani—kila aina ya maombi!

# 3



## AINA YA MAOMBI

*Kwanza kabisa basi, naomba dua, sala, maombi na sala za shukrani zitolewe kwa Mungu kwa ajili ya watu wote.*

Kwa ajili ya wafalme na wote wenye mamlaka, ili tupate kuishi maisha ya utulivu na amani pamoja na uchaji wa Mungu na mwenendo mwema.

Jambo hili ni jema na lampendeza Mungu Mwokozi wetu.

*1 Timotheo 2:1-3*

Kama tunavyoona katika maandiko haya, tunafaa kuomba kila aina ya maombi tukijiombea na kuwaombea wengine pia.

Hebu tuangalie aina tofauti ya maombi ambayo tunafaa kuomba tunapoanza kujifunza kuomba kwa moyo bila kukoma.

### ***Ombi la kujitolea***

Umkabidhi BWANA njia yako, pia umtumaini, naye atafanya.

*Zaburi 37:5 (UNION)*

Kwanza kuna maombi ya kujitolea ambapo tunayatoa maisha yetu na kumkabidhi Bwana. Tunafanya hivyo tunapompa hofu zetu. Kama tunavyoambiwa katika 1 Petro 5:7 "...Mwekeeni matatizo



yenu yote, maana yeye anawatunzeni.”

Wakati tunakumbwa na hofu ya mambo na shida ambazo zinatishia kutuungamiza, tunahitaji kuomba:

“Bwana, mimi sitaubeba mzigo huu wa matatizo na kuukubali unitese na kunizuia kukutumikia. Baba ninaomba sasa hivi kwamba utanipa nguvu na kuniwezesha kufanya yale ambayo umeniitia kufanya hata kama nitayafanya nikiwa mwenye hofu. Ninakuwekea shida hii, chochote kiovu, kibaya au cha kuchukiza, ambacho shetani anajaribu kunionyesha kwamba kitanitokea. Ni shauri lako, si langu kwa maana nitafanya yale uliyoniambia na nikuachie hayo mengine.”

Iwapo tutaomba mara tu hofu inapojitokeza— basi tutaona hofu hiyo ikishindwa kwa nguvu za Mungu.

Shida ni kwamba, si hofu kubwa ambazo hututatiza sana. Mara nyingi hofu ndogo ndogo ambazo hutuandama usiku na mchana ndizo hutuibia uzima na furaha yetu kama vile mbweha wadogo wanavyoharibu ambao huharibu mizabibu (Wimbo 2:15).

Ndio maana, unapohisi hofu, hata iwe ndogo kiasi gani, unahitaji kuomba, “Bwana, sitaishi kwa hofu. Badala yake, ninakukabidhi maisha yangu na ninakuomba ushindi juu ya jambo hili ambalo linajaribu kunitesa na kunizuia kuishi maisha kamili ambayo unatamani niishi na kutimiza mpango wako mzuri na mkamilifu.”

Iwapo tutaomba hivyo kwa moyo na dhati, basi Bwana ataheshimu maombi yetu na kujitoa kwetu na atatimiza sehemu yake ya kutuweka huru.

### ***Maombi ya Kujitakasa au Kujiweka Wakfu***

Kwa hiyo, ndugu zangu, maadam Mungu ni mwenye huruma nyingi, nawasihi kwa moyo wote: jitoleeni nafsi zenu kwa Mungu kama tambiko iliyo hai, takatifu na yenye kupendeza. Hii ndiyo

njia yenu halisi ya kumwabudu.

*Warumi 12:1*

Wakati tunapokitoa kitu kwa Mungu katika maombi, hilo huwa ombi la kuweka wakfu. Tunapofanya hivyo tunasema, “Bwana, ninakupatia pesa zangu, wakati wangu, nia yangu”— chochote kile tunachomtolea Bwana.

Mtume Paulo anatumia katika maandiko haya tuteo, na kuweka wakfu miili yetu kwa Bwana, viungo vyote vya miili yetu vipate kumtumikia, ambayo ndio njia yetu halisi ya kumwabudu.

Sisi pia huomba ombi la kuweka wakfu wakati tunapowatoa watoto wetu kwa Bwana, tukiahidi “...kuwalea katika kumcha na kumheshimu Mwenyezi—Mungu.” (Waefeso 6:4).

Jinsi tunavyoweka wakfu maisha yetu, pesa na mali yetu, nia na miili yetu, jamii na watoto wetu kwa Mungu, ndivyo pia tunafaa kutoa na kuiweka wakfu midomo yetu—na kufanya hivi kunatuongoza katika aina ifuatayo ya maombi.

### ***Ombi la Sifa na Ibada***

Basi, kwa njia ya Yesu, tumtolee Mungu dhabihu ya sifa daima, yaani sifa zinazotolewa na midomo inayoliungama jina lake.

*Waebrania 13:15*

Nafikiri sote tunafahamu sifa na ibada. Sifa ni kuyarudia mema ambayo Mungu amefanya. Ni kusema hadithi ya mema aliyotufanyia. Ibada ni kumsujudu. Ni kutambua “Kustahili” kwake. Ni kumtambua yeye na utukufu wake. Hii ndio sababu mwandishi wa kitabu cha Waebrania anatumia kwamba tunafaa kuwa tunamsifu na kumwabudu Mungu kila wakati. Kama tulivyoona, ombi la sifa na ibada linafaa kuwa kama kupumua, mchana na usiku, kila wakati. Tunafaa kuwa na shukrani kwa

Mungu kila wakati. Tukitambua, tukikiri na kulitukuza jina lake katika maombi, sifa na ibada.

### ***Ombi la Shukrani***

Na muwe na shukrani katika kila hali. Hayo ndiyo anayotaka Mungu kwenu katika kuungana kwenu na Kristo Yesu.

*1 Wathesalonike 5:18*

Mara tu baada ya kutuambia katika 1 Wathesalonike 5:17 tuombe bila ya kukoma, Mtume Paulo anatumshukuru Mungu katika kila jambo. Haijalishi kinachoendelea katika maisha yetu kwa maana hili ndilo kusudi la Mungu kwa ajili ya maisha yetu.

Jinsi maombi yanavyopaswa kuwa mtindo wa maisha yetu, ndivyo shukrani inapaswa kuwa sehemu ya maisha yetu.

Kumshukuru Mungu hakupaswi kuwa jambo ambalo tunafanya mara moja kwa siku tunapoketi chini na kujaribu kufikiri mambo yote mema ambayo Mungu ametufanyia, na kusema kwa udhaifu, "Asante Bwana."

Hiyo ni dini, jambo ambalo tunafanya kwa sababu tunafikiri kuwa Mungu anatumhitaji tumfanyie. Shukrani ya kweli huendelea kububujika kutoka kwenye moyo ambao umejaa shukrani na sifa kwa Mungu kwa sababu ya utukufu wake na matendo yake. Si jambo tunalofanya ili atutimizie hitaji fulani, tupate kibali, tupate ushindi, au ili tuhitimu kuweza kupata baraka.

Aina ya shukrani ambayo Mungu Baba anatamani kutoka kwetu ni ile ambayo imechochewa na Roho Mtakatifu ndani yetu ambaye anatumvuta tumweleze Bwana yale tunayohisi katika roho zetu.

Shukrani ya kweli ni ile iliyoelezwa na mwandishi wa Zaburi aliposema: "Mshukuruni Bwana wa mabwana, kwa maana

huruma zake na fadhili zake zadumu milele—” (Zaburi 136:3)!

### ***Maombi Katika Roho***

Lakini ninyi, wapenzi wangu, endeleeni kujijenga kikamilifu katika imani yenu takatifu. Salini kwa nguvu ya Roho Mtakatifu.

*Yuda 20*

Tulikuwa tayari tumeona katika waefeso 6:18 kwamba hatufai kuomba maombi ya kila aina bila kukoma tu, bali jinsi tunavyoambiwa na Yuda, maombi yetu yanafaa kuwa “katika Roho Mtakatifu.”

Ni Roho Mtakatifu wa Mungu ndani yetu ambaye hutuchochea na kutuongoza kuomba. Badala ya kusubiri, mimi na wewe tunahitaji kujifunza kujitoa kwa Roho Mtakatifu mara tu tunapohisi mwongozo wake. Hii ni sehemu ya kujifunza kuomba kila aina ya maombi kila wakati, popote tulipo, hata tunapokuwa tukifanya chochote.

Mwito wetu unafaa kuwa ule wa tenzi ya kitambo iliyosema, “Kila nitakapohisi Roho Mtakatifu akinichochea moyoni, nitaomba.”

Iwapo tunajua tunaweza kuomba wakati wowote, mahali popote, basi hatutahisi tunalazimika kungoja hadi wakati na mahali maalum ili tuweze kuomba.

### ***Ombi la Kukubaliana***

Tena nawaambieni, wawili miongoni mwenu wakikubaliana hapa duniani kuhusu jambo lolote la kuomba, Baba yangu wa mbinguni atawafanyia jambo hilo.

Kwa maana popote pale wanapokusanyika wawili au watatu kwa jina langu, mimi nipo kati yao.”

Kuna nguvu katika kukubaliana.

Biblia inatuambia kwamba iwapo Bwana yu pamoja nao, mtu mmoja anaweza kuwapiga elfu moja, na wawili wanaweza kuwapiga elfu kumi. (Kumbukumbu 32:30). Lakini nguvu hii inapatikana tu wakati tunakuwa katika makubaliano na wenzetu—pamoja na Bwana.

Ni wazi kwamba hatuwezi kugombana na wenzetu kila wakati na kisha tukubaliane katika maombi kuhusu hitaji fulani na tutarajie kwamba “Ombi la kukubaliana” litakuwa na nguvu – ndivyo tunavyoonywa katika 1 Petro 3:7 (UNION): “Kadhalika nyinyi waume, kaeni na wake zenu kwa akili; na kumpa mke heshima, kama chombo kisicho na nguvu; na kama warithi pamoja wa neema ya uzima, kusudi kuomba kwenu kusizuiliwe.”

Vivyo hivyo, hatuwezi kunungunika na kumsengenya mhubiri wa neno wiki nzima na kisha tumwendee kwa maombi kuhusu shida fulani ambayo imetukumba na tutarajie kwamba ataomba ombi la makubaliano pamoja nasi. Kwa nini?

Kwa sababu tayari hatumo katika makubaliano - na wenzetu na Mungu.

Unajua ni kwa nini Mungu anaheshimu maombi ya kukubaliana? Ni kwa sababu anajua kuwa si jambo rahisi kwetu kutembea na kuishi katika makubaliano na wengine. Mungu anamheshimu mtu yeyote ambaye amejitoa kufanya hivyo.

Mimi na wewe tukikubaliana na wenzetu na Mungu pia, basi maombi yetu yatakuwa yenye nguvu na uwezo zaidi.

### ***Maombi ya Pamoja***

“Hawa wote walikusanyika pamoja kusali...”

*Matendo 1:14*

Kuna nguvu kubwa katika maombi ya pamoja, ambayo ni aina mojawapo ya ombi la kukubaliana kama inavyodhihirika katika mstari huu tuliosoma.

Katika kitabu cha Matendo, tunasoma kwamba watu wa Mungu walikuja, “wakakusanyika pamoja” (Matendo 2:1, 46, 4:24, 5:12, 15:25).

Katika wafilipi 2:2, tunaambiwa na mtume Paulo, “Ikamilisheni furaha yangu kwa kuwa na nia, moja, kusudi moja, na upendo mmoja.”

Iwapo tutayafuata maneno haya na tuishi na kukubaliana na wenzetu na Mwenyezi Mungu, tutaona matokeo ya ajabu kama walivyoona wafuasi wa kwanza katika kitabu cha Matendo.

## ***Maombezi***

Kwanza kabisa, basi naomba dua, sala, maombi na sala za shukrani zitolewe kwa Mungu kwa ajili ya watu wote.

*1 Timotheo 2:1*

Kumfanyia mtu maombezi, ni “Kusimama pengoni kwa ajili yake.” Ni kumwomba mbele ya kiti cha enzi cha Mwenyezi Mungu.

Katika Warumi 8:26,27, tunaambiwa na mtume Paulo kwamba Roho Mtakatifu hutuomba kulingana na mapenzi ya Mungu.

Katika Waebrania 7:25 tunasoma kwamba Yesu “...anaweza daima kuwaokoa kabisa wote wanaomwendea Mungu kwa njia yake, maana yeye anaishi milele kuwaomba kwa Mungu.”

Mwishowe, Paulo anatumiza hapa katika 1 Timotheo 2:1, tuwafanyie maombezi watu wote. Kumaanisha kwamba tunafaa kuwaomba watu wote kila mahali.

Maombezi ni mojawapo ya njia muhimu kabisa katika kuendeleza huduma ya Yesu aliyozanzisha hapa duniani.

### ***Ombi la Kukimya***

...Bwana yu hekaluni Mwake; dunia yote na iwe kimya mbele zake.

*Habakuki 2:20*

Mimi huita aina hii ya maombi, “kumngoja Bwana.”

Daudi alijua kuhusu kumngoja Bwana kama tunavyoona katika Zaburi 27:4 alipoandika: “Jambo moja ninalitamani, kwamba nikae nyumbani mwa Bwana siku zote za maisha yangu, niutazame uzuri wa Bwana na kutafakari katika hekalu mwake takatifu.”

Ni muhimu sana kujifunza kumngoja Bwana kwa sababu watu wengi hawaelewi kwamba ni muhimu kufanya hivyo katika maombi.

Maombi si jambo tunalofanya tu, bali pia ni kuwa na nia ya kungoja. Maombi si kumzungumzia Mungu kila wakati—ni kumsikiza pia.

### ***Ombi la Mahitaji ya Kibinafsi***

Msifadhaike juu ya jambo lolote; lakini katika kila jambo mjulisheni Mungu haja zenu, kwa kusali na kuomba pamoja na kushukuru.

*Wafilipi 4:6*

Ombi la kibinafsi ni kumwomba Mungu akutane na mahitaji yetu.

Mimi husema kwamba ombi kuu kabisa ambalo mtu yeyote anaweza kuomba ni ombi ninaloliita, “Ombi la Nisaidie”. “Mungu nisaidie, nisaidie, Ee Mungu nisaidie!”

Mimi huliomba sana.

Wakati mwingine mimi huamka usiku wa manane kwenda kujisaidia, na sina shida yoyote; bali ninajikuta ninaomba, “Ee Mungu, nisaidie, nisaidie mimi!” Ninaamini ni Roho Mtakatifu aniongezeaye kuomba hivyo.

Ombi hili la “Mungu nisaidie” ni ombi lenye nguvu sana. Iwapo mimi na wewe tumefika mahali ambapo hakuna la ziada tuloweza kufanya, tunaweza kuomba hivi.

Ombi lingine la kibinafsi ni lile ninaloliita, “Bwana, Nakuhitaji.”

Tunaweza kuona mabadiliko makubwa katika maisha yetu iwapo tutaacha kujaribu kufanya kila kitu kwa nguvu zetu wenyewe.

Mithali 3:5-7 inatuambia: “Mtegemee Bwana kwa moyo wako wote, naye anainyosha njia yako. Usiwe mwerevu machoni pako, bali mche na kumwabudu Bwana na kuachana na maovu.”

Usingoje mpaka wakati utakapokuwa umeshindwa na kutambua kwamba huwezi kushinda peke yako ndipo umkimbilie Mungu akusaidie. Tambua kabla hata hujajaribu, kwamba huwezi lolote kwa nguvu zako. Mtegemee Mungu kabisa.

Jifunze kuomba hivi: “Bwana, siwezi kufanya jambo hili, lakini wewe unaweza kwa kunitumia mimi. Ninakutegemea na kukutazamia, nikiwa na tumaini ndani yako kwa moyo wangu wote. Nisaidie Bwana, kwa maana ninakuhitaji.”

Ombi hilo dogo linatosha kukuwezesha kushinda hali mbaya mno maishani. Kutambua kuwa Mungu ndiye msaada wetu huchukua muda mfupi sana lakini kunaweza kutusaidia kushinda kushindwa katika hali za maisha yetu ya kila siku—hasa tunapogundua kwamba bila Bwana hatuwezi chochote.

Unaposema, “Bwana, ninakutegemea, nisaidie tafadhali,” umeomba ombi la kibinafsi—nalo lina nguvu. Haya ndiyo maombi tunayofaa kuomba tunapowasilisha hitaji la aina yoyote



kwa Mungu. Tunafaa kuwa huru kuzungumza na Bwana kuhusu kitu chochote maishani mwetu. Kumbuka, anatupenda sana—naye anaguswa na kujali juu ya chochote kinachotuhusu.

### ***Weka Mambo ya Kwanza Kwanza!***

Walipokuwa safarini, waliingia katika kijiji kimoja na mwanamke mmoja, aitwaye Martha, alimkaribisha nyumbani kwake. Martha alikuwa na dada yake aitwaye Maria; huyu aliketi karibu na Yesu akisikiliza mafundisho yake.

Lakini Martha alikuwa anashughulika na mambo mengi. Basi, akamwendea Yesu, akamwambia, “Bwana, hivi hujali kwamba dada yangu ameniacha nishughulike peke yangu? Mwambie basi, anisaidie.”

Lakini Bwana akamjibu, “Martha, Martha, unahangaika na kusumbuka kwa mambo mengi. Kitu kimoja tu ni muhimu. Maria amechagua kitu bora zaidi ambacho hakuna mtu atakayemnyag’anya.”

*Luka 10:38-42*

Pengine kufikia sasa umeanza kugundua kwamba una maisha mazuri ya maombi kuliko ulivyofikiria. Umeona kuwa ingawa ni muhimu kuwa na mahali na wakati maalum ambapo unamwomba Bwana, hasa unapoanza siku yako, kuna nguvu kuu unapokuwa katika maombi nyakati zote.

Njia ya kuunda maisha yenye nguvu ya maombi ni kwa kuendelea kuwa katika uwepo wa Bwana. Kama wafuasi wa Yesu, tunafaa kuunda msingi wa maisha yetu katika jambo hili.

Ikiwa tutakaa katika uwepo wa Bwana kwa muda kabla ya kuanza siku yetu, na kisha tuendeleo tukiutambua uwepo huo mchana kutwa, tutaona matokeo ya ajabu kila siku.

Iwapo unafikiri huna wakati wa kutosha kushiriki na Bwana,

tumia kanuni hii: jiambie; “Jinsi ninavyoendelea kuwa na shughuli nyingi, ndivyo ninavyohitaji kutumia muda mwingi na Bwana.” Kwa sababu jinsi nilivyo na mengi ya kufanya, ndivyo ninavyohitaji msaada zaidi kutoka kwake.

Ukiwa mtu wa shughuli shughuli kama Martha kiasi cha kwamba huna wakati wa kukaa na Bwana, basi wewe una shughuli kupita kiasi. Unahitaji kuwa kama Maria na ujifunze kuachana na mambo mengine yasiyo ya maana sana ili upate kukaa miguuni pa Bwana na kujifunza kutoka kwake.

Ukifanya hivyo, basi utapata funguo za ufalme kutoka kwake!

# 4



## FUNGUO ZA UFALME

*Nitakupatia funguo za ufalme Wa Mbinguni.*

*Mathayo 16:19*

Yesu alipofika pande za Kaisarea Filipi, aliwauliza wanafunzi wake, “Watu wanasema Mwana wa Mtu kuwa ni nani?”

Wakamjibu, “Wengine wanasema kuwa ni Yohana mbatizaji, wengine Eliya, wengine Yeremia au mmojawapo wa manabii.”

Yesu akawauliza, “Na ninyi je, mwasema mimi ni nani?”

Simoni Petro akajibu, “Wewe ndiwe Kristo, Mwana wa Mungu aliye hai.”

*Mathayo 16:13-16*

Wakati Petro aliposema hayo kumhusu Yesu, kwamba yeye ni Kristo, Mwana wa Mungu aliye hai, alikuwa anaachilia imani iliyokuwa moyoni mwake kupitia kwa kinywa chake.

Tunahitaji kuelewa kwamba tunathibitisha imani iliyo mioyoni mwetu kupitia kwa maneno tunayozungumza na vinywa vyetu, kama tunavyosoma katika Warumi 10:10 (UNION): “Kwa maana kwa moyo mtu huamini hata kupata haki, na kwa kinywa hukiri hata kupata wokovu.”

Hii ndio maana maombi yana umuhimu sana. Maana tunayathibitisha tunayoyaamini ndani yetu tunapoanza kuyakiri wazi wazi.

Hii ndio sababu pia kukariri maandiko ni muhimu. Tunapofanya hivyo, tunadhibitisha mambo katika ulimwengu wa kiroho kwa maneno tunayoyazungumza katika ulimwengu huu halisi. Na mwishowe, yale ambayo yamejithibitisha katika ulimwengu wa kiroho yatajionyesha katika ulimwengu huu.

Tunafaa kuwa tunalikiri neno mara kwa mara, tukisema mambo kama haya: “Baba, ninakuamini. Ninaamini unanipenda sana kiasi cha kumtuma Yesu afe msalabani kwa ajili yangu.

“Ninaamini umenijaza na Roho Mtakatifu. Ninaamini una mpango mzuri kwa ajili ya maisha yangu, na unanitia nguvu nitimize mpango huo.

“Ninaamini upako wako u juu yangu ili niwawekee wagonjwa mikono nao wapate kuponywa, na pia kuyakemea mapepo, nayo yapate kutoroka.

“Ninaamini kulingana na neno lako, kila kitu ninachokifanya na mikono yangu kitafanikiwa.”

Tunafaa kuendelea hivi, tukiamini katika mioyo yetu na tukikiri kwa vinywa vyetu yale Mungu anayosema kutuhusu katika neno lake.

Kitu kimoja ambacho amesema ni kwamba hajatupatia roho ya woga, bali roho ya nguvu na upendo na moyo wa kiasi. Hivyo, tunafaa kukiri kila wakati, “Sitaogopa!”

### ***Imani Itashinda!***

Yesu akasema, “Heri wewe Simoni mwana wa Yona, kwa maana si binadamu aliyekufunulia ukweli huu, ila Baba yangu aliye mbinguni.

*Mathayo 16:17,18*

Je, ni mwamba gani ambao Yesu anazungumzia katika andiko hili? Anazungumzia mwamba wa imani. Anamwambia Simoni Petro kwamba imani ambayo ameionyesha itatumiwa na Bwana kulijenga kanisa lake na milango ya kuzimu haitalishinda. *Mst 18*

Hii inamaanisha kwamba milango ya kuzimu haitaweza kumshinda mtu anayetembea kwa imani.

Hofu hutoka kuzimu. Ndio maana Yohana anatuambia, "...hofu ina dhiki..." (1 Yohana 4:18) lakini wakati hofu inakabiliwa na imani, basi haiwezi kushinda.

### ***Funguo za Ufalme***

"Nitakupa funguo za Ufalme wa mbinguni; kila utakachofunga duniani, kitafungwa pia mbinguni; kila utakachofungua duniani, kitafunguliwa pia mbinguni."

*Mathayo 16:19*

Hapa Yesu alikuwa anasema hivi, "Chochote kinachoendelea kule mbinguni, ninakupatia nguvu na mamlaka ya kutekeleza hapa duniani."

Huku ndiko kutimilika kwa maombi ambayo Yesu alikuwa amewafundisha wanafunzi wake katika Mathayo 6:10: "Ufalme wako uje, mapenzi yako yatendeke; hapa duniani kama huko juu mbinguni."

Baadaye katika Mathayo 18:18 Yesu alipeana nguvu zizi hizi za kufunga na kufungua, kwa wafuasi wake wote alipowambia, "Nawaambieni kweli, mtakachofunga duniani kitafungwa mbinguni, na mtakachokifungua duniani kitafunguliwa mbinguni."

Kile Yesu alikuwa anawaambia ni kwamba walikuwa na nguvu na

mamlaka ya kutumia funguo alizokuwa amewapa ili kutekeleza mapenzi ya Mungu hapa duniani jinsi yalivyotendeka mbinguni.

Ninaamini kuwa funguo alizompa Petro na wanafunzi wengine - na sisi pia-zinaweza kuwa zinazungumzia aina ya maombi ambayo tumezungumzia hapo awali.

### ***Maombi ya Moyoni Yana Nguvu***

Sala ya mtu mwema ina nguvu ya kutenda mengi.

Eliya alikuwa binadamu kama sisi. Aliomba kwa moyo mvua isinyeshe, nayo haikunyeshwa nchini kwa muda wa miaka mitatu na miezi sita.

Kisha akaomba tena, mvua ikanyesha kutoka angani na nchi ikatoa mazao yake.

*Yakobo 5:16-18*

Katika idara yoyote, ni nani mwenye nguvu na mamlaka? Ni yule mwenye funguo. Funguo hufanya nini? Hufunga na kufungua. Hii ndio maana ya maandiko yale yanayohusu “kufunga na kufungua” – ni kama kutumia funguo kufunga na kufungua kifuli.

Wakati wa kumfanyia mtu maombezi, tunafungua baraka juu ya mtu huyo. Tunafungua mlango wa kuzimu ambao umemfunga. Ndivyo ilivyo tunapoomba ombi la shukrani. Tunafungua baraka juu ya maisha yetu.

Basi sisi sote tumepewa funguo za ufalme. Tukiwa na funguo hizo za maombi, tuna nguvu za kuwezesha mapenzi ya Mungu yafanyike hapa duniani kama yanavyofanyika mbinguni. Hii ni fursa nzuri tena kuu!

Ndio maana shetani anataka kutudanganya tufikiri kuwa maisha yetu ya maombi hayana nguvu—ili tuache kujaribu badala ya kutumia funguo hizo kushinda ufalme wake wa giza.

Usiache shetani akudanganye kuhusu maisha yako ya maombi. Anza kumtambua Mungu, ukimwitia katika maombi—kila aina ya maombi—ukitegemea kwamba maombi yako ya moyo yanafanya kazi kwa sababu hujitegemei bali unaiweka imani yako ndani ya Mungu.

### ***Maombi ni Kuitisha***

Msiwe na wasiwasi juu ya chochote, bali kwa sala na maombi, mjulisheni Mungu mahitaji yenu.

*Wafilipi 4:6*

Tuliangalia maandiko haya tulipozungumzia maombi ya kibinafsi.

Neno “kuomba” lililotumika hapa linamaanisha kutaja kwa Mungu haja zetu zifahamike wazi wazi. Neno lingine lenye maana sawa na “kuomba” kama lilivyotumika katika mstari huu ni kuitisha.

Je kuitisha ni kufanya nini? Ni kuomba au kutaka kitu ambacho ingawa unastahili kuwa nacho, bado hujakipata. Mfano mzuri ni wakati kamanda wa jeshi anaweza kuitisha mavazi na vifaa vingine kwa ajili ya askari wake. Kama kamanda wa majeshi yale, anastahili kupata vitu vile, lakini kwanza ni lazima ajaze fomu ya kuviitisha kwa kuvitaja.

Bwana amenionyesha kwamba tunapomba, tunaitisha kile ambacho tayari ametutengea wakati wa mahitaji.

Hebu nikupatie mfano kutoka katika hali ya maisha ya kawaida. Mimi na wewe tunaweza kuwa tumeweka pesa katika benki. Lakini kwetu sisi kuweza kuzipata na kuzitumia, ni lazima tujaze kijikaratasi cha kuziitisha au tumwandikie mtu mwingine cheki ili aweze kuzipata na kuzitumia kufanya jambo fulani.

Hivi ndivyo mume wangu ambaye ndiye msimamizi wa fedha

katika huduma yetu hufanya. Iwapo meneja wa kitengo fulani atakuwa anahitaji kiasi fulani cha pesa, hata ingawa pesa hizo zimewekwa kwa ajili ya matumizi ya kitengo hicho, ni lazima kwanza ajaze fomu kueleza kiasi cha pesa anachohitaji na kusudi ambalo zinanuiwa kutumikia.

Hii ndio maana ya maombi—ni fomu ya mbinguni tunayomwandikia Mungu ili atupe kile tunachohitaji katika maisha na katika huduma.

### ***Omba Katika Jina la Yesu***

Ninyi pia mna huzuni sasa; lakini nitawajieni tena, nanyi mtajaa furaha mioyoni mwenu, na furaha hiyo hakuna mtu atakayeiondoa kwenu.

Siku hiyo hamtaniomba chochote. Kweli nawaambieni, chochote mtakachomwomba Baba kwa jina langu, atawapeni.

*Yohana 16:22,23*

Biblia inatufundisha kwamba Mungu anajua kila kitu kutuhusu sisi. (Zaburi 139:1-6.) anajua tunachohitaji kabla yetu kumwomba. (Mathayo 6:8,32.) Hata hivyo, ameamuru tumwombe.

Hatuwezi kuvipokea vitu tunavyohitaji kwa kuvitamani tu. Yafaa kuelewa kwamba kusema, “Natamani ningekuwa na pesa zaidi” au “Natamani ningeponywa kichwa changu” au “Natamani ningeshi bila hofu” si ombi litakalo kubalika mbinguni.

Kulingana na yale tunayosoma katika Yakobo 1:5-8, tunahitaji kuomba kile tunachohitaji kwa imani, tukiamini kwamba tunapokea, kwa maana tumeomba kutoka kwenye ghala la baraka alizotuwekea Mwenyezi Mungu.

Katika maandiko yaliyo kwenye Yohana 16, ambayo Yesu aliwaambia wanafunzi wake kabla ya kwenda msalabani,



anatuambia wazi kwamba tunapoomba, zaidi ya kuamini kwamba tumepokea, tunafaa kuomba katika jina lake.

Hii haimaanishi kwamba kila neno tunalosema linafaa kukamilishwa na msemo, "Katika jina la Yesu." Tusipokuwa waangalifu, tunaweza kujawa na dini kiasi cha kwamba kila neno linalotoka vinywani mwetu linaishia na "Haleluya," au "Bwana Asifiwe" au "Katika Jina la Yesu." Tukifanya hivi, nguvu ilioko katika maneno haya inapotezwa.

Yesu hakusema tufanye hivi. Alikuwa anazungumzia kutumia mamlaka ya jina lake, kama alivyotumia tufanye, ili mapenzi yake yafanyike hapa duniani kama yafanyikavyo juu mbinguni. Alikuwa anazungumzia kupeleka ombi rasmi kwa baba tukitumia sahihi ya mwanaye kutimiza yote tunayohitaji kuendeleza ufalme wa Mungu.

Katika huduma yetu, wafanya kazi wana muda wa likizo. Hii ni haki yao. Lakini hata kama ni haki yao, hawawezi kupewa ruhusa kabla yao kuomba rasmi ruhusa ya kwenda likizoni.

Sote tuna urithi ambao tumewekewa mbinguni na ambao umenunuliwa na kulipiwa kwa damu ya Yesu iliyomwagika. (Waefeso 1:11,12.) Ni haki yetu. Lakini shida ni kwamba hatujakuwa tukifanya maombi rasmi ya kutosha.

Iwapo mfanyakazi katika huduma yetu anampa Dave ambaye ndiye msimamizi wa fedha maombi hayo ya kwenda likizoni, naye mtu huyo anakosa kupewa ruhusa ya kuondoka, yeye humjia Dave baada ya muda na kumuuliza, "Je, ulipoteza ombi langu? Nitapata ruhusa ya likizo yangu lini?"

Wakati tumewasilisha ombi letu kwa Mungu katika jina la Yesu, na hatujapokea yale ambayo tumeomba kwa imani, basi tuna haki ya kwenda mbele ya Baba na kumuuliza, "Bwana, umelisahau ombi langu?" kufanya hivi si kukosa heshima, ni imani. Ni kumheshimu Bwana kwa sababu inaonyesha kwamba tunamtarajia atimize neno lake kwa sababu yeye ni mwaminifu.

## *Tumia Jina la Yesu*

Mpaka sasa hamjaomba chochote kwa jina langu. Ombeni nanyi mtapata ili furaha yenu ikamilike.

*Yohana 16:24*

Yesu alituamrisha tuombe kwa jina lake ili tupokee na furaha yetu ikamilike.

Nina hakika kwamba sababu moja kuu ya kukosa furaha katika maisha ya Wakristo wengi leo ni kwa sababu ya kukosa kuomba. Moja ya sababu ya kukosa kuomba ni kwa sababu watu wanajaribu kufanya mambo kwa nguvu zao—mambo ambayo wangepokea kuyaomba na kumwuliza Mungu awafanyie na kuwasaidia kufanya.

Yesu aliwaambia wanafunzi wake kwamba baada yake kufufuliwa kutoka kwa wafu, basi wangepokea nguvu na mamlaka ambayo walikuwa hawajawahi kufurahia kabla ya kufa na kufufuka kwake.

Alisema, “Wakati huo ukifika, hamtaniomba chochote, lakini mtaweza kwenda kwa Baba moja kwa moja, naye atawapa chochote mtakachotaka—katika jina langu.”

Je inamaanisha nini kuomba katika jina la Yesu?

Kulingana na mstari wa 24, kuomba katika jina la Yesu ni kuja kwake Mungu Baba na kumbukumbu ya yale yote ambayo Yesu amekamilisha.

Mojawapo kati ya sababu ambazo sisi ni wadhaifu sana ni kwa sababu sisi humwendea Mungu na kumbukumbu ya utu wetu. Shida ya kuwa na kumbukumbu kama hii ni kwamba wakati wowote tunapojihisi kuwa na hatia mbele zake, tunafikiri kwamba hatuna lolote ambalo tunaweza kufanya kumvuta Mungu kwetu ili atushughulikie.

Biblia inasema kwamba mbele ya Mwenyezi Mungu, haki yetu sisi wenyewe ni kama nguo iliyotiwa unajisi. (Isaya 64:6) Kwa hivyo hakuna chochote ndani yangu na wewe kinachoweza kutuwakilisha kwa Mungu Baba ila damu ya Yesu pekee.

Ndio maana nimesisimka sana kwa sababu ya kitabu changu kiitwacho Neno, Jina na Damu. Ninazungumzia mambo haya katika kitabu hicho.

Wakati tunapokuja mbele ya kiti chake cha neema, tukifunikwa na damu ya Yesu, tukiomba kwa imani kulingana na neno lake na katika jina la Mwanaye Yesu Kristo, tunaweza kujua kwamba amejibu maombi yetu. Si kwa sababu tunastahili au sisi ni wakamilifu, au kwa sababu Mungu ana deni letu, lakini ni kwa sababu anatupenda na anataka kutupatia yote tunayohitaji kufanya kazi ambayo ametuitia.

Kuna nguvu katika jina la Yesu. Katika jina la Yesu, kila goti litapigwa mbinguni, duniani, na chini ya dunia. (Wafilipi 2:10). Kwa nguvu za jina hilo, mimi na wewe leo tunaweza kuwawekea wagonjwa mikono na wapate kuponywa, tutoe mapepo nayo yatoroka, na tufanye matendo ya Yesu na hata zaidi kwa ajili ya utukufu wa Mwenyezi Mungu. (Marko 16:17, 18; Yohana 14:12).

Yesu ametununulia urithi mtukufu kwa kuimwaga damu yake. Sasa sisi ni warithi pamoja naye (Warumi 8:17). Kila kitu ambacho amekipata huko mbinguni kwa sababu ya kujitoa kwake, tumewekewa sisi. Tuna funguo za ghala hilo, funguo za maombi.

Hatuhitaji kuishi kwa hofu na ukosefu. Hebu tuanze kutumia funguo za ufalme kufungua milango hiyo ili baraka za mbinguni zipate kutunyeshea kwa utukufu wa Mungu, ili mpango wa Mungu mtimilifu upate kutendeka hapa duniani kama kule mbinguni, na furaha yetu ipate kukamilika.

# MWISHOWE

Hofu haitoki kwa Mungu. Inatoka kwa shetani.

Nia inayokubalika ambayo Mkristo anafaa kuwa nayo kuhusu hofu ni hii: “Hofu haitoki kwa Mungu, nami sitaivumilia au kuiacha itawale maisha yangu! Nitaikabili hofu, kwa sababu ni roho kutoka kuzimu ambayo imekuja kunitesa.”

Mimi husema mara kwa mara kwamba hofu ndiyo roho ambayo shetani hutumia kujaribu kuwazuia watu wa Mungu wasiwe chini ya uongozi wa Bwana wa kweli, Yesu Kristo.

Ninaamini Mungu hufanya kazi ndani yetu kwa upole akittoa kutoka kwa utumwa hadi kwenye uhuru wake. Biblia imejaa maagizo yatuambiayo, “Usiogope.” Kama tulivyosema hapo mwanzoni, matukio katika maisha yangu yamenifundisha kwamba “Usiogope” humaanisha “Usikimbie.”

Ninakuhimiza uendelee mbele, na hata ikihitajika, “Tenda hata ukiwa na hofu.” Usitoroke na kuogopa hofu, badala yake, ikabili kwa maombi na imani.

Kumbuka, Mungu anataka kukukomboa kutokana na hofu zote.

H – HABARI YA

O – UONGO

F – INAYOFANANA

U - UKWELI

**Sehemu ya 2**

**Maandiko**

## MAANDIKO YA KUSHINDA HOFU



...Msiogope! Kaeni imara! Leo mtaona jinsi Mwenyezi Mungu atakavyowakomboa...

*Kutoka 14:13*

Tazameni, Mwenyezi Mungu Mungu wenu ameiweka nchi hii mbele yenu. Haya! Ingieni, mkaimiliki kama Mwenyezi—Mungu, Mungu wa wazee wenu alivyowaambia. Msiogope wala msifadhaike!

*Kumbukumbu 1:21*

Muwe imara na hodari, wala msiwaogope wala kutishwa nao, maana Mwenyezi—Mungu, Mungu wenu ndiye anayekwenda pamoja nanyi. Yeye hataacha kuwasaidia na hatawatupa

*Kumbukumbu 31:6*

Kumbuka kuwa mimi nimekuamuru uwe imara na hodari. Usiogope wa usifadhaike kwa kuwa mimi Mwenyezi—Mungu Mungu wako, niko pamoja nawe popote uendapo.

*Yoshua 1:9*

Basi usiogope, mimi nipo pamoja nawe. Usifadhaike, mimi ni Mungu wako. Nitakuimarisha na kukusaidia; nitakulinda kwa mkono wangu wa ushindi.

Mimi ndimi Mwenyezi—Mungu, Mungu wako, ndimi ninayetegemeza mkono wako. Mimi ndimi ninayekuambia: "Usiogope, nitakusaidia."

*Isaya 41:10,13*

Mwenyezi Mungu aliyewaumba enyi watu wa Yakobo, yeye aliyewafanya enyi watu wa Israeli, asema: msioCOPE, maaana mimi nimewakombo; nimewaita kwa jina nanyi ni wangu.

Mkipita katika mafuriko, mimi nitakuwa pamoja nanyi; mkipita katika mito, haitawashinda nguvu. Mkitembea katika moto, hamtaunguzwa; mwali wa moto hautawaunguza.

*Isaya 43:1,2*

Kwa maana, Roho mliyempokea si Roho mwenye kuwafanya ninyi watumwa na kuwatia tena hofu; sivyo, bali mmempokea Roho mwenye kuwafanya ninyi watoto wa Mungu, na kwa nguvu ya huyo Roho, sisi tunaweza kumwita Mungu, "Aba," yaani "Baba!"

*Warumi 8:15*

Msiwaogope adui zenu, bali muwe hodari daima, na hiyo itawathibitishia kwamba wao watashindwa, nanyi mtashinda kwani Mungu mwenyewe ndiye anayewapeni ushindi.

*Wafilipi 1:28*

Msiwe na hofu kuhusu lolote, bali kwa sala na dua pamoja na kushukuru, mjulisheni Mungu mahitaji yenu. Na amani ya Mungu ipitayo ufahamu wote, itailinda na kuihifadhi mioyo yenu ndani ya Yesu Kristo.

*Wafilipi 4:6,7*

Kwa maana Mungu hakitupa Roho wa kutufanya tuwe waoga, bali alitupa Roho wa kutujalia nguvu, upendo na nidhamu.

*2 Timotheo 1:7*

Msiwe watu wa kupenda fedha; toshekeni na vile vitu mliyvo navyo. Mungu mwenyewe amesema: "Sitakuacha kamwe, wala sitakutupa." Ndiyo maana tunathubutu kusema: "Bwana ndiye msaada wangu, sitaogopa. Binadamu atanifanya nini?"

*Waebrania 13:5,6*

Palipo na upendo hapana uoga; naam, upendo kamili hufukuza uoga wote. Basi, mtu mwenye uoga hajakamilika bado katika upendo, kwani uoga huhusikana na adhabu.

*1 Yohana 4:18*



# OMBI LA KUKABILIANA NA HOFU



Ee Bwana, nikomboe kutokana na hofu.  
Nisaidie niwe na uhodari na ushujaa mtakatifu.

Nisaidie, "Nisiogope", bali niweze  
kusonga mbele na kupokea yote ambayo  
umenitayarishia.

Nisaidie nifahamu jinsi unavyonipenda,  
kwa sababu upendo kamili hufukuza hofu yote.  
Katika jina la Yesu, Amen.

# OMBI LA KUWA NA UHUSIANO WA KARIBU NA BWANA



Iwapo hujawahi kumkaribisha Yesu, mfalme wa amani, awe mwokozi wako, ninakualika ufanye hivyo sasa hivi. Omba ombi hili, na kama unamaanisha kwa moyo wako, basi utapokea maisha mapya katika Kristo.

*Baba,*

*Uliupenda ulimwengu sana, Ukamtoa mwana wako wa pekee afe msalabani ili yeyote atakayeamini asiangamie bali awe na uzima wa milele.*

*Neno lako linasema ya kwamba tunaokolewa kwa neema kupitia imani na hii ni karama kutoka kwako. Hakuna chochote tunachoweza kufanya ili tufaidi kuokolewa.*

*Ninaamini na kukiri kwa kinywa changu ya Kwamba Yesu Kristo ni mwana wako. Ninaamini alikufa msalabani kwa ajili yangu na kubeba dhambi zangu zote, na hivyo akanilipia deni la dhambi zangu. Ninaamini katika moyo wangu kwamba ulimfufua Yesu kutoka kwa wafu.*

*Ninakuomba unisamehe dhambi zangu. Ninamkiri Yesu kuwa Bwana. Kulingana na neno lako, nimeokolewa na nitaishi milele pamoja nawe! Asante Baba, ninashukuru sana. Katika jina la Yesu, Amen.*

Tazama Yohana 3:16, Waefeso 2:8,9, Warumi 10:9,10; 1 Wakorintho 15:3,4; 1 Yohana 1:9; 4:14-16; 5:1,12,13.

# KUHUSU MWANDISHI



Joyce Meyer amekuwa akifundisha Neno la Mungu tangu mwaka wa 1976 na amekuwa katika huduma tangu mwaka wa 1980. Kabla ya hayo alikuwa Mchungaji msaidizi katika kanisa la Life Christian Centre huko St. Louis, Missouri, na alianzisha na kushirikisha mpango wa mkutano wa kila wiki ambao ulijulikana kama “Uzima ndani ya Neno (Life in the Word)”. Baada ya muda wa miaka mitano, Bwana alikamilisha mpango huo, na kumuongoza kuanzisha huduma yake na akaiita “ Life in The Word, Inc.”

Sasa, kipindi chake cha Life in The Word hupeperushwa kupitia Redio na Televisheni na husikika na kuonekana na mamilioni ya watu kote Marekani na ulimwenguni. Kanda zake husikizwa kimataifa, na husafiri sana akifundisha neno kupitia huduma ya Life in The Word.

Joyce na mumewe Dave, ambaye ndiye msimamizi wa shughuli za huduma ya Life In the Word, wameoana kwa muda zaidi ya miaka 34. Wanaishi St. Louis Missouri, na wana watoto wanne. Watoto wote wameoa na kuolewa na wote wanafanya huduma pamoja na Dave na Joyce.

Akiamini kwamba wito wake ni kuwastawisha waumini katika neno la Mungu, Joyce anasema “Yesu Alikufa kuwaweka huru waliosetwa, na Wakristo wengi hawana ushindi au wanashindwa katika maisha yao ya kila siku.” Alijipata katika hali hii miaka mingi iliyopita na baada ya kupata uhuru wa kuishi maisha ya ushindi kupitia Neno la Mungu, Joyce sasa hutembea hapa na pale akiwa amejiandaa kuweka huru waliosetwa na kubadili hali ya huzuni kuwa ya furaha. Anaamini kwamba kila mtu anayeishi

maisha ya ushindi apaswa kuwasaidia wengine kuishi maisha kama hayo. Maisha yake ni ya uwazi, na mafundisho yake ni rahisi na ya kueleweka yanayoweza kutumika katika maisha ya kila siku.

Joyce amefundisha kuhusu uponyaji wa hisia na mafundisho mengine yanayoandamana na hayo katika mikutano yake yote nchini Amerika, akiwasaidia maelfu. Amenakili zaidi ya kanda za redio 225 na zaidi ya kanda 70 za Video. Ameandika zaidi ya vitabu 45 kusaidia mwili wa Kristo kuhusiana na mada tofauti tofauti.

Mafunzo yake kuhusu “Uponyaji wa Hisia” yanachukua zaidi ya masaa 23. Mafundisho hayo yanajumuisha kanda kama “Ujasiri”, “Urembo badala ya Majivu”; “Kumilki hisia zako”; “Uchungu, Chuki, na Kutosamehe”; “Mzizi wa Kukataliwa”; na kanda ya dakika 90 ya vifungu vya Biblia na muziki iitwayo “ Uponyaji wa moyo uliovunjika”